Mkombozi Centre for Street Children

Mradi wa Uimarishaji Jamii

JARIDA

Taarifa ya Robo Mwaka
(Julai - Septemba 2005)



Tathmini ya mwisho ya mradi wa Uimarishaji Jamii

Tathmini ya mwisho wa mradi wa Uimarishaji Jamii ilifanywa na Salma Maoulid hapo tarehe 1 hadi 15 Agosti 2005. Tathmini ilijumuisha kupitia nyaraka za mradi, majadiliano na wafanyakazi wa mradi, watoto wa Mkombozi na wawakilishi kutoka kwenye jamii. Wawakilishi hao wa jamii walikuwa Kaka/dada mkubwa, Kaka/ dada wadogo, watu kutoka serikalini, wasuluhishi wa migogoro na waimarishaji rika. Mtathimini pia alifanya mazungumzo na asasi za kiraia, viongozi wa kidini, watoto wa mitaani na wananchi kwa ujumla.

Yafuatayo ni miongoni mwa mapendekezo muhimu ambayo yamejitokeza katika tathmini hii ya mwisho:

- Ili kuhakisha mahusiano mazuri kati ya mradi wa Uimarishaji Jamii na idara nyingine Mkombozi inapaswa ifuate mpango unaoruhusu maingiliano baina ya idara.

- Kuboresha utumiaji wa kitabu chenye taarifa za watoa huduma kwenye jamii Mkombozi mara kwa mara iwatumie watoa huduma wanaopatikana kwenye kitabu hicho ili kuboresha majukumu yao kijamii.

- Ili kuongeza uwajibikaji kwa wanajamii, Mkombozi iwafahamishe wanajamii kuwa hatimaye itawakakabidhi wanajamii wenyewe uendeshaji wa shughuli zao za kijamii.

Mafunzo ya utumiaji kitabu cha watoa huduma yawa kifungua macho

Mafunzo yaliyofanyika karibuni ya utumiaji kitabu cha watoa huduma yaliwakusanya zaidi ya wasuluhishi 50 kutoka kwenye jamii. Lengo la mafunzo lilikuwa ni kuamsha ufahamu kwa wanajamii juu ya huduma zilizopo kwenye maeneo yao. Wasuluhishi walitaka kufahamu namna gani taarifa hizi zitawasaidia katika kazi zao.

Uchunguzi uliofanywa wakati wa mafunzo umeonyesha wanajamii wanaweza kutambua huduma zinazotolewa kwenye maeneo yao (mfano Bw Domisian Skaya ana gari, Parokia ya Katoliki Umbwe inayo mashine ya kusaga). Wanajamii walionyesha huduma zinazopatikana katika maeneo yao wanazithamini na kuzishukuru hata zile ambazo ni za kulipia. Kwa ujumla washiriki wa warsha waliafiki kwamba kuna huduma nyingi za kijamii ambazo kama zitatumika vizuri zitasaidia jamii.

Kaka/dada wadogo wanasemaje kuhusu mradi wa kaka/dada mkubwa

Ni wazi sasa mpango wa kaka/dada mkubwa umeanza kuzaaa matunda. Baadhi ya mafanikio yanaelezwa hapa chini na kaka/dada wadogo*:

"Mkubwa wangu amenisaidia vikubwa sana. Hatimaye ninapata msaada maalum. Sijui ningelikuwa wapi leo."
~ Asha Makamba

"Ninaelewa ninataka kuwa nani katika maisha."
~ Erick Hamisi

"Ninafahamu zaidi na nina uwezo wa kukabiliana na majaribu ya kimapenzi kutoka kwa wavulana. Ahsante kwa mkubwa wangu."
~ Maggie Mkapa

"Mkubwa wangu yuko nami siku zote na anahakikisha naenda shule. Ninafikiria kuhusu masomo yangu."
~ Yussuf Nyerere

"Hatimaye nitafanya mtihani wangu wa darasa la saba. Nimejifunza namna ya kukabilina na wavulana wajanja."
~ Marie Maro

***Kumbuka:** Majina yamebadilishwa ili kutunza siri.

Waimarishaji Rika wazungumzia juu ya Elimu

Muelimishaji Rika kutoka shule ya msingi Kimanganuni anaelezeea hadithi inayomhusu baba yake:

"Elimu ni msingi wa maendeleo kwa kila mtu katika hii dunia. Babu yangu alimpeleka baba yangu shuleni. Alipokuwa hasomi shule alikuwa mchafu lakini baada ya kuanza shule alibadilika na kuwa msafi. Pia alianza kufuga sungura na kuku nyumbani. Wakati mmoja alikuwa na sungura 21 na kuku 30. Aliwauza wakati bado akiwa shule, na babu alimfungulia baba akaunti benki. Baba yangu sasa ni mkulima, amejenga nyumba na anatulipia ada za shule na mahitji mengine ya msingi. Kama angekuwa hajaelimika hata sisi tusingekwenda shule. Hivyo nawashauri wanarika wenzangu kufuata mfano huu wa baba yangu."

Sauti za watoto kwenye uchaguzi wa mwaka 2005

Masikio ya watu yameelekezwa katika kufuatilia uchaguzi ambao unatarajiwa kufanyika tarehe 30 Oktoba 2005. Wanasiasa ambao wanataka nyadhifa wanafanya kampeni za kisiasa kuwashawishi wananchi wawapigie kura wao na vyama vyao. Mnamo tarehe 24 Septemba, Sylvanus Alloyce, Katibu wa kitaifa wa Baraza la watoto ambaye ni kijana wa Mkombozi alikutana na wanachama 24 kutoka wilaya 5 za mkoa wa Kilimanjaro. Katika mkutano huo Sylvanus aliwaeleza matokeo ya mkutano wa kitaifa kuhusu manifesto ya watoto uliofanyika Dodoma tarehe 29 Juni 2005.

Manifesto hiyo inaelezea mambo ambayo watoto wanayapa kipaumbele katika miaka mitano ijayo. Wawakilishi wa watoto wa kila wilaya walipewa taarifa na kuzisambaza katika wilaya zao kwa viongozi wa vijiji, watendaji kata, wagombea udiwani, ubunge na urais. Wawakilishi wa watoto waliwakumbusha wagombea uongozi wajibu wao kwa watoto; kwa mfano, kuhakisha watoto wanapewa nafasi ya kutosha ya kuendeleza uwezo wao.

Mabango, vipeperushi na vijitabu vya manifesto ya watoto kutoka KULEANA vimekuwa vikisambazwa kote mkoani Kilimanjaro. Mwana kampeni Bwana Shambe Saggaf anasema: “Nina furahi kuwataarifu kwamba nimesambaza kijitabu cha manifesto ya watoto kwa mgombea urais kwa tiketi ya CCM, mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro, Mkurugenzi wa Manispaa ya Moshi na mgombea ubunge wa Moshi Mjini. Nimewapa wakati wakifanya mkutano uwanja wa Mashujaa na wakati wa kikao maalum kwenye ukumbi wa CCM.”

Wasuluhishi wa migogoro wasuluhisha kesi katika maeneo yao

Baada ya mafunzo kutolewa kwa wasuluhishi wa migogoro katika miezi mitatu iliyopita, wasuluhishi wamesuluhisha migogoro mingi katika maeneo yao na wanataarifu juu ya mafanikio katika kutatua migogoro; kwa mfano:

- Manushi ndoo, watoto walikuwa wanaiba mahindi katika shamba la jirani. Ingawa wazazi walitaka watoto wachapwe mbele ya jamii, kesi ilisuluhishwa wakati mlalamikaji alipoamua kuwasamehe watoto kwa kuwa walikuwa wameelewa kuiba ni makosa.

- Huko Rau baba wa kambo alikuwa akimchapa mtoto mara kwa mara kwa sababu tu mtoto hakuwa wake na kwa kuwa mtoto "alikuja na mama yake". Kesi ilitatuliwa baada ya usuluhishi wa kamati.

- Huko Shauri Moyo, watoto walipoteza vitabu walivyoazimana. Wazazi wa watoto wakaingizwa katika kesi hiyo, walitishiana na kusema vitabu lazima vilipwe au kurudishwa. Kamati ya usuluhishi ilishauri kwamba vitabu vinunuliwe na hivyo kesi ikawa imetatuliwa.

~ P.O. Box 9601 Moshi, Tanzania ~ Tel: (255) 27 2754793 ~ Fax: (255) 27 2753410 ~
~ info@mkombozi.org ~ http://www.mkombozi.org ~